





Huyu anaitwa Bi Simu.
Mtazame vizuri!




Bi Simu ana simu tano.
Asubuhi, yeye
huzipanga simu zake
tano mezani.




Kila simu inatumika kwapigia watu tofauti. Simu ya rangi ya manjano ni ya kuwasiliana na familia yake.




Nayo ile ya rangi nyeupe, ni ya kuwasiliana na wenzake anaofanya nao kazi.




Bi Simu huitumia ile ya rangi nyekundu kuwasiliana na watu anaowadai!




Ile ya rangi ya waridi ni
ya kuwasiliana na
marafiki zake wa
karibu.



Kuna ile ya kizambarau. Bi Simu huitumia hii kuwasiliana na wanaohitaji msaada wake.




Bi Simu hufurahia watu
wanapofurahi.
Hapendi ugomvi wala
vita.




Asipokuwa kazini, Bi Simu huwaalika watoto ukumbini kwake. Wao hutazama runinga na kupata mawaidha.



Bi Simu anawahurumia wanyonge. Huwatembelea wagonjwa na wazee nyumbani kwao.



Kila apitapo, watu hupiga mayowe wakimwita, "Bi Simu! Bi Simu!"



Naye hufurahia na kusema, "Mimi ni Bi Simu. Nazitumia simu zangu kuwasiliana na wote." Huyo ni Bi Simu na simu zake tano!